**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA MKUTANO MAALUM KUHUSU MWENENDO WA HALI YA MAZINGIRA NCHINI

**UKUMBI WA MIKUTANO WA JAKAYA KIKWETE – DODOMA**
**09 SEPTEMBA, 2024**

- ***Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira);***
- ***Mhe. Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Wahe. Wakuu wa Mikoa wote mliopo;***
- ***Wahe. Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo;***
- ***Mhandisi Cyprian Luhemeja, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira);***
- ***Viongozi wa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi;***
- ***Prof. Davis George Mwamfupe, Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma;***
- ***Wahe. Wakuu wa Wilaya mliopo;***
- ***Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri mliopo;***
- ***Maafisa Waandamizi na Wataalamu wa Mazingira;***
- ***Viongozi wa Dini;***
- ***Wadau wa Mazingira;***
- ***Waandishi wa habari;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...!**

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki,***

Tumekutana katika Mkutano huu muhimu kwa lengo kuu la kujadili kwa pamoja kuhusu mwenendo uharibifu wa mazingira nchini na kuona hatua zinazoweza kuchukuliwa kukabiliana na changamoto zilizopo. Aidha, tutapata fursa ya kujadili kuhusu masuala muhimu katika uhifadhi wa mazingira hususan biashara ya kaboni, uchumi wa buluu pamoja mfumo mzima wa usimamizi wa mazingira. Ni matarajio yangu kuwa majadiliano na maazimio ya Mkutano huu yatatusaidia kusukuma mbele ajenda ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Kipekee, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada kubwa anazofanya kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Ameendelea kusimamia na kutoa miongozo mahsusi katika kuhifadhi mazingira na maliasili ili kuchangia katika Pato la Taifa, pamoja na kushiriki katika jitihada za kitaifa na kimataifa za kutafuta ufumbuzi wa changamoto za mazingira Duniani.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Suala la usimamizi na uhifadhi wa mazingira ni kipaumbele katika maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo, Taarifa ya Nne ya Mazingira ya Mwaka 2024 inaonesha kuwa hali ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira nchini hairidhishi. Nchi yetu bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali za mazingira ambazo kwa kiasi kikubwa zinatokana na tabiawatu, naomba nitilie mkazo chache zifuatazo:

(i) Ukataji wa miti hovyo na uharibifu wa misitu, ambapo takwimu zinaonesha ongezeko kubwa la uharibifu wa misitu kutoka hekta 372,816 mwaka 2019 hadi hekta 469,420 mwaka 2023. Kwa takwimu hizi ina maana kwamba tunapoteza wastani wa hekta 24,151 kila mwaka. Uharibifu huu umechangiwa kwa sehemu kubwa na shughuli za binadamu zisizo endelevu ikiwemo utegemezi mkubwa wa nishati ya kuni na mkaa; uvunaji wa

rasilimali misitu usioendelevu; kilimo kisicho endelevu na ufugaji holela usiozingatia uwiano wa idadi ya mifugo na maeneo ya malisho;

(ii) Uchafuzi wa Mazingira, hususan kutokana na utupaji taka hovyo au kiholela (taka ngumu, majitaka, plastiki na sumu) hususan katika maeneo ya mijini. Takwimu pia zinaonesha kuwa, takriban kiasi cha tani milioni 7 za taka ngumu huzalishwa hapa nchini kwa mwaka, ambapo wastani wa 50% tu ya taka hizo hukusanywa na kutupwa ipasavyo. Sehemu ya taka inayobaki hutupwa hovyo, hali inayochangia uchafuzi wa mazingira na magonjwa ya milipuko;

(iii) Uharibifu wa vyanzo vya maji/Uvamizi wa ardhi oevu: Ukataji miti, kilimo katika maeneo ya vyanzo vya maji; kutozingatia matumizi bora ya ardhi na ufugaji holela huchangia katika uharibifu wa mazingira kwa kukausha vyanzo vya maji na upotevu wa bioanuwai. Hivi leo tunashuhudia migogoro kati ya wakulima na wafugaji, uvamizi wa wanyama kama tembo na makundi makubwa ya mifugo katika maeneo kama Bonde la Mto Ruaha, Kilombero, Rufiji, Ruvu na Malagarasi, na

(iv) Matumizi ya Nishati chafu: Takwimu za Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, zinaonesha kuwa 82% ya nishati inayotumika kwa ajili ya kupikia inatokana na kuni na mkaa. Matumizi ya nishati chafu hupelekea ukataji wa miti ili kukidhi mahitaji makubwa ya nishati na pia huathiri afya za akina mama wanaotumia nishati chafu kupikia. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiye kinara wa ajenda ya matumizi ya Nishati safi ya kupikia kitaifa, Barani Afrika na duniani kote. Katika kufanikisha ajenda hii hapa nchini, mkakati uliopo unalenga kuwa 80% ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimazingira, Serikali yetu imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa Sera; Kanuni; Mikakati; programu za upandaji miti; kampeni za usafi na hasa mijini na kwenye fukwe; kuhamasisha utunzaji wa mazingira kupitia vyombo vya habari; mashindano ya mikoa na halmashauri katika usafi, ushiriki katika siku ya mazingira duniani na programu ya jenga kesho iliyo bora (BBT). Pamoja na hatua zote hizo, Taarifa ya 4 ya Hali ya Mazingira nchini pamoja na taarifa zilizopita (2008,2014,2019) zinaonesha uharibifu bado ni mkubwa. Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mfano, imekuwa ikiandaa Taarifa ya Hali ya Mazingira kwa kuzingatia Kifungu cha 175 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191. Taarifa ya Nne ya Hali ya Mazingira (2024) imeandaliwa, na itajadiliwa kwa kina katika mkutano huu. Ni imani yangu kuwa Makala Mjongeo pia imetoa mwanga wa hali ya uhifadhi wa mazingira na kutuwezesha kubuni namna tutakavyojipanga kukabiliana na changamoto za kimazingira. Taarifa zilizopita ziliandaliwa mwaka 2008, 2014 na 2019. Licha ya jitihada zote hizo, kwa ujumla hali ya mazingira nchini siyo nzuri! Hii inatokana na sababu mbalimbali na baadhi ya sababu ninazoziona, ni zifuatazo:

- Sheria kinzani. Mfano, mkaa kuwa chanzo cha mapato cha TFS. Hii inahamasisha utoaji wa vibali vya kukata miti;
- Kasi ya upandaji miti ni ndogo kuliko kasi ya ukataji miti;

- Vitalu vya miche ya miti havitoshelezi mahitaji;
- Miti iliyopandwa haitunzwi (haimwagiliwi wakati wa kiangazi, inachomwa moto na inaliwa na mifugo);
- *Modernization* ya ufugaji bado ni mwendo mrefu;
- Kuna tuhuma kuwa wafanyabiashara ya mkaa baadhi yao ni wafanya maamuzi na wana maslahi binafsi;

- Mazoea ya kutupa taka hovyo bado yapo na udhibiti/sheria za kuzuia utupaji taka ni dhaifu;
- Miundombinu ya ukusanyaji taka ikiwemo Madampo ya kisasa, magari ya kuzolea taka haitoshelezi;
- Viwanda vya kurejeleza taka (recycling) ni vichache mno

- Kilimo na ufugaji vinagongana na mahitaji ya kutunza mazingira. Mfano, kilimo cha mpunga Mbarali kinakinzana na mahitaji ya wanyamapori na kulinda vyanzo vya Ruaha mkuu;
- Mahitaji ya kilimo na ufugaji yanashindana na mahitaji ya maeneo yaliyotengwa kwa uhifadhi;
- Teknolojia za kijani hazipatikani kwa urahisi na zinapopatikana ni ghali. Mfano, transition from hydro-carbons as source of energy;
- Wenye kipato kidogo kutomudu teknolojia za kijani. Serikali kama ya Tanzania ina uwezo mdogo wa kutoa ruzuku.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***
Ni jukumu la mkutano huu kuainisha namna bora ya kufikia matokeo tarajiwa kwa kutafuta majibu ya changamoto za kimazingira zilizopo. Mathalan, katika changamoto ya uimarishaji wa mfumo wa usimamizi wa mazingira nchini, ninatarajia washiriki wa mkutano huu kupendekeza namna bora ya kuhuisha mfumo huo. Kwa jinsi nionavyo mimi, tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuweka sera na kanuni, isipokuwa kuna mapungufu ya kisheria kuhusu nguvu na wigo wa Mamlaka ya usimamizi wa mazingira (NEMC). Na hapa ningependa Mkurugenzi Mkuu wa NEMC aweke bayana mapungufu hayo ili washiriki waweze kuchangia katika kutafuta ufumbuzi wake. Vilevile, maelekezo yanayolenga kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa mazingira nchini yamekuwa yakitolewa mara kwa mara na viongozi wakuu wa nchi, lakini utekelezaji unaonekana kuwa hafifu katika ngazi ya Mikoa, Halmashauri na vijiji.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***
Biashara ya kaboni ni fursa katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, biashara hiyo haifahamiki kwa walio wengi na hivyo kushindwa kutumia fursa hiyo kikamilifu. Ni matumaini yangu kuwa wataalamu kutoka Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni (National Carbon Monitoring Centre) watatupatia elimu kuhusu biashara hii, na namna bora ambayo wananchi wetu wanaweza kutumia ili kulinda na kuvuna rasilimali za misitu. Aidha, wataalamu watusaidie kutupa elimu kuhusu wajibu wa Jumuiya ya Kimataifa kwa nchi kama Tanzania ambazo zina Masinki makubwa ya Kaboni (carbon sinks), ikiwa ni pamoja na eneo kubwa la bahari na maziwa, ardhi oevu na eneo

kubwa la hifadhi lililotengwa. Pia, wataalamu wetu watufundishe kuhusu mikataba bora ya hewa ya kaboni iweje kwa maana ya mapato na teknolojia kutoka nchi zilizoendelea ambao ndiyo wazalishaji wakubwa wa hewa ya kaboni.

Kwenye programu ya mkutano huu kuna nafasi ya kupata wasilisho kuhusu dhana ya uchumi wa buluu ambayo imejikita katika kukuza uchumi kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za maji, sambamba na mikakati wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mawazo yangu, eneo hili bado linahitaji utafiti wa kutosha unaolenga kubaini rasilimali nyingi zinazopatikana katika maji na menejimenti yake. Mfano wa rasilimali hizo ni pamoja na gesi asili, madini, viumbe hai, matumbawe n.k.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Ni matarajio yangu kuwa mkutano huu utasaidia kuainisha na kupendekeza njia zifaazo kuimarisha mfumo wa usimamizi wa mazingira pamoja na kutatua changamoto zilizopo. Nawaomba watoa mada kujikita katika kuwawezesha na kuwahamasisha washiriki kuibua suluhu ya changamoto za kimazingira zilizopo.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Kwa niaba ya Serikali nalishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP) pamoja na Wadau wengine kwa mchango wao katika kufanikisha Mkutano huu muhimu, lakini zaidi kuleta mtazamo na uzoefu wa kimataifa katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira na fursa za mashirikiano.

Kwa umuhimu wa ajenda ya mkutano huu, namwelekeza Waziri wa Nchi – Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuwasilisha taarifa ya mkutano huu na mapendekezo yatakayotolewa na washiriki mapema iwezekanavyo. Pia ni matarajio yangu kuwa washiriki wote wakiwemo Wahe. Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na wengine, watashiriki hadi mwisho wa mkutano huu bila kuondoka kwa kuwa Mgeni Rasmi ameondoka.

Baada ya kusema hayo, ninayo heshima kutamka kuwa Mkutano Maalum Kuhusu Mwenendo wa Hali ya Mazingira Nchini umefunguliwa rasmi.

**Asanteni kwa kunisikiliza!**